**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimwa Spika,** napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa fursa ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, ni jambo la furaha na heshima kubwa kwa Kamati yangu kuwasilisha Taarifa yake kuhusu Ofisi ya Rais (Muungano) tukiwa tunaadhimisha miaka 53 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Natoa pongezi kwa Serikali zote mbili kwa kuhakikisha kwamba Muungano huu unadumu na unaendelea kuwa na faida kwa pande zote mbili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016**,** naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Katiba na Sheria ina jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imeendelea kutekeleza jukumu hili la kuisimamia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) toka kuundwa kwa Kamati hii Mwezi Januari 2016 na ndani ya miezi 15 iliyopita Kamati imetembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo iliyo chini ya Ofisi hii pamoja na kupokea Taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi hii, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 tarehe 22 Machi

2017. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Raisi(Muungano) Tarehe 02 Aprili, 2017 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) pamoja na kuchambua Taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kufanya ulinganisho kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Rais ina mafungu mawili (2) ya bajeti kama ifuatavyo;

i) Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais
ii) Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais

**Mheshimiwa Spika, Taarifa** hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makubwa manne (4) yafuatayo:-

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; na Utekelezaji wa mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
iii) Maoni na Ushauri wa Kamati

## 2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 98 (1) inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Katika kutekeleza masharti ya Kanuni hiyo, Kamati ya Katiba na Sheria ilitembelea, kukagua na kupokea Taarifa ya utekelezaji wa mradi Na.6309 –ujenzi wa Ofisi na

Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu- Unguja ulio chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais tarehe 22 Machi 2017.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Tisa Sabini na Tatu , Themanini na Tatu Elfu, Mia Nne Arobaini na Nane (10,973,083,448.00) kwa ajili ya Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Nane (8,000,000,000.00) ni fedha za ndani na Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tisa Sabini na Tatu, Themanini na Tatu Elfu Mia Nne na Arobaini na Nane (2,973,083,448.00) ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2017 Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Thelathini na Saba, Laki Tano Sabini na Saba Elfu, Mia Tano Sitini na Nane (1,237,577,568.00) zilikuwa zimepokelewa. Fedha hii ni sawa na asilimia 11 ya fedha yote ya miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge mwezi Mei, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, mradi namba 6309 ambao ni ujenzi wa Makazi na Ofisi ya Makamu wa Rais Tunguu, Unguja katika Mwaka wa fedha 2016/2017 ulitengewa Shilingi Milioni Mia Saba (700,000,000.00).

**Mheshimiwa Spika**, kwa sababu Kamati ya Katiba na Sheria inasimamia masuala yote ya Muungano kwa ujumla, ilionekana ni vema kukagua miradi mingine ya Maendeleo iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37) iliyopo Unguja na Pemba pamoja na Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) zilizopo Pemba. Taarifa za ukaguzi wa Miradi hii ya Maendeleo zipo katika Taarifa mahsusi za Kamati kuhusu Wizara/Ofisi hizi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha kwamba Miradi mbalimbali ya maendeleo kama ile ya MIVARF (Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Financing) ulio chini ya Waziri Mkuu na ile ya TASAF iliyo chini ya Ofisi ya Rais inaendelea kuwafikia na kuwanufaisha wananchi wengi walioko Tanzania Zanzibar. Wakati wa ziara kwenye miradi ya ujenzi wa masoko na barabara Unguja na Pemba, Kamati ilijionea jinsi miradi hii ilivyo na faida kubwa kwa wananchi wengi wa maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika**, miradi mingine chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais inayohusiana na masuala ya mazingira inasimamiwa na Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Baadhi ya miradi hii inatekelezwa Unguja na Pemba.

**Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni yafuatayo ya jumla kuhusu miradi iliyokaguliwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kama ifuatavyo;

**MRADI NA.6309-UJENZI WA OFISI NA MAKAZI YA MAKAMU WA RAIS, UNGUJA ;**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu kwa mara ya kwanza, ulitengewa fedha katika bajeti ya maendeleo ya mwaka wa fedha 2008/2009. Lengo la mradi huu lilikuwa ni kukidhi mahitaji ya makazi na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kupata Ofisi inayoweza kutumiwa na watumishi wote wa ofisi hiyo waliopo Unguja na kupata makazi ya kudumu ya Mheshimiwa Makamu wa Rais. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 mradi huu ulitengewa Shilingi Milioni Mia Saba (Shs.700, 000,000.00). Katika mwaka ujao wa Fedha 2017/2018 , mradi huu umetengewa Shilingi Milioni Mia Tatu (300,000,000.00).

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais umeshakamilika kwa kiasi kikubwa na mkandarasi amewasilisha hati ya kukamilisha ujenzi (Final Account) na muda wa matazamio umeshaisha. Kamati inatoa rai kwa Mkandarasi na Ofisi ya Makamu wa Rais kukamilisha mapungufu yaliyoonekana katika mradi na kuhakikisha kwamba changamoto zote zilizoonekana zinafanyiwa kazi na kukamilika katika mwaka ujao wa fedha.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA OFISI YA MAKAMU WA RAIS KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016 Kamati ilikutana Dodoma Tarehe 02 Aprili, 2017 kwa ajili ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilizingatia mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Mwezi Mei, 2016 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi mwezi Machi, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 ili kujua vipaumbele vya kibajeti katika Mwaka wa Fedha Ujao.

## i) OFISI BINAFSI YA MAKAMU WA RAIS (FUNGU 26)

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, Fungu 26, ilidhiinishiwa Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Sita Arobaini na Tisa, Laki Moja Themanini na Nne Elfu (3,649,184,000.00). Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne Tisini na Tisa na Laki Nane (2,499,800,000.00) ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Arobaini na Tisa, Laki Tatu Themanini na Nne Elfu (1,149,384,000.00) ni kwa ajili ya mishahara.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2017 Fungu 26 ilipokea kiasi cha Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tano Thelathini na Tatu , Laki Mbili na Arobaini na Sita Elfu, Mia Mbili Sitini na Tatu (3,533,246,263/= ) kutoka Hazina sawa na asilimia 97 ya Bajeti yote. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nane Arobaini na Nane, Laki Nane Sabini na Tisa Elfu, Mia Mbili Sitini na Tatu na Senti Tisini (2,848,879,263.90) ni za matumizi ya mengineyo sawa asilimia 113.9 ya bajeti ya matumizi mengineyo na Shilingi Milioni Mia Sita Themanini na Nne, Laki Tatu Sitini na Saba Elfu (684,367,000) ni za mishahara sawa na asilimia 59.5 ya bajeti ya mishahara.

**Jedwali Na.01: Mchanganuo wa Fedha Zilizoidhinishwa na Kupokelewa Chini ya Fungu 26 katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Hadi Kufikia Machi,2017**

| | **Fedha Zilizoidhinishwa** | **Fedha Zilizopokelewa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Kawaida | Sh. 2,499,800,000 | Sh. 2,848,879,263.90 | 113.9 |
| Mishahara | Sh. 1,149,384,000 | Sh. 684,367,000 | 59.5 |
| Maendeleo | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **3,649,184,000** | **3,533,246,263.90** | **97** |

**ii) OFISI YA MAKAMU WA RAIS – (FUNGU 31)**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu 31, iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tatu Themanini na Sita, Laki Sita Tisini na Tisa Elfu, Mia Nne na Arobaini na Nane (20,386,699,448.00). Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Nne Kumi na Tatu, Laki Sita Kumi na Sita Elfu na (9,413,616,000.00) ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Tisa Sabini na Tatu, Themanini na Tatu Elfu ,Mia Nne na Arobaini na Nane (10,973,083,448.00) ni fedha za miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2017, Ofisi ilipokea Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Saba Tisini na Tatu, Laki Nne Tisini na Tatu Elfu, Mia Saba Thelathini na Saba (7,793,493,737.18) sawa na asilimia 38.2 ya fedha iliyoombwa. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tano Hamsini na Tano, Laki Tisa Kumi na Sita Elfu, Mia Moja na Sitini na Nane (6,555,916,168) zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo jumla ya Sh. Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Thelathini na Saba, Laki Tano na Sabini na Saba Elfu, Mia Tano Sitini na Nane na Senti Hamsini (1,237,577,568.50/=) ambayo ni sawa na asilimia 11 ya fedha yote ya miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge.

## 3.1 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, Kamati imeridhika kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni ya Kamati yaliyotolewa mwezi Mei 2016, kama ilivyoelezwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kwenye Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais zilizowasilishwa mbele ya Kamati. Katika Taarifa ya Kamati iliyosomwa katika Bunge hili Mwezi Mei, 2016 kamati ilitoa maagizo, maoni na ushauri kwa Ofisi ya Makamo wa Rais ambayo kwa ujumla yamezingatiwa na kufanyiwa kazi na Ofisi ya Makamu wa Rais katika mwaka huu wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** moja kati ya maagizo ya Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais ilikuwa ni kufanyia kazi mapungufu yaliyoonekana katika mradi Na. 6389 kuhusu Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais lililopo Luthuli, Dar es Salaam. Kamati imepokea Taarifa ya utekelezaji kuhusu mradi wa jengo hili na inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kurekebisha kasoro zote zilizoonekana katika mradi huu bila

kutumia gharama nyingine za ziada kama zile za kuwalipa washauri elekezi (Consultants) kama ilivyokusudiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Badala yake Kamati inashauri Wakala wa Majengo (TBA) washughulikie mapungufu yaliyoonekana kwa gharama nafuu ili kuokoa fedha za walipa kodi wa Tanzania.

## 4.0 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) imepanga kutekeleza malengo mbalimbali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kuhusu uratibu wa masuala ya Muungano. Katika kuhakikisha kwamba malengo haya yanafanikiwa Ofisi ya Makamu wa Rais imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

i) Kuratibu vikao vya kamati ya pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar vya kushughulikia masuala ya Muungano pamoja na changamoto zilizojitokeza;

ii) Kuelimisha Umma kuhusu Muungano;

iii) Kuratibu utekelezaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii kwa faida ya pande zote mbili za Muungano;

iv) Kuratibu ushirikiano kwa kuhimiza Wizara na Taasisi zisizo za Muungano zenye majukumu yanayoshabihiana kwa pande zote, kukutana mara mbili (2) kwa mwaka ili kuimarisha katika masuala yasiyo ya Muungano.

## 5.0 MAPITIO YA BAJETI OFISI YA MAKAMU WA RAIS FUNGU 26 na 31 KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inaonyesha maombi ya jumla ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Fungu 26) na Ofisi ya Makamu wa Rais (Fungu 31) kulingana na vipaumbele vilivyowekwa.

## 5.1 OFISI YA MAKAMU WA RAIS (FUNGU 26)

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2017/18 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaomba jumla ya Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Tisa Kumi na Nne, Laki Sita na Nane Elfu. (Sh.4,914,608,000.00) ambapo Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Saba Hamsini na Nne , Laki Tisa Sitini na Tano Elfu (3,754,965,000.00) ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Hamsini na Tisa, Laki Sita Arobaini na Tatu Elfu (1,159,643,000.00) ni kwa ajili ya mishahara. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 26 ukilinganisha na kiasi kilichoombwa mwaka huu wa fedha (2016/2017).

**Mheshimiwa Spika**, fedha hizi zinategemewa kumwezesha Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na maagizo ya Mheshimiwa Rais pamoja na kufanikisha majukumu mengine muhimu ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais.

## 5.2 OFISI YA MAKAMU WA RAIS (FUNGU 31)

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Ofisi ya Makamu wa Rais inaomba jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mbili, Laki Tisa Themanini na Nane Elfu, Mia Nne Thelathini na Saba (15,002,988,437.00) ili kutekeleza majukumu yake mbalimbali. Kati ya Fedha hizo, Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Mbili Kumi na Nne, Laki Tano Thelathini na Sita Elfu (8,214,536,000.00) ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Saba Themanini na Nane, Laki Nne Hamsini na Mbili, Mia Nne Thelathini na Saba (6,788,452,437.00) ni fedha za miradi ya maendeleo. Katika fedha ya matumizi ya kawaida inayoombwa, Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Moja na Ishirini, Laki Tatu na Ishirini na Nne Elfu (3,120,324,000.00) ni fedha za mishahara na Shilingi Bilioni Tano, Milioni Tisini na Nne, Laki Mbili na Kumi na Mbili Elfu (5,094,212,000.00) ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa bajeti unaonyesha kwamba, ukomo wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Fungu 31) umekua ukishuka toka mwaka wa Fedha 2015/2016 kwa kiasi kikubwa. Katika mwaka wa Fedha 2016/2017 ukomo wa bajeti ulishuka kwa wastani wa Shilingi Bilioni Kumi na Saba (17,000,000,000.00) ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2015/2016. Ukomo wa bajeti kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 umeshuka kwa wastani wa Shilingi Bilioni Tano (5,000,000,000.00) ukilinganisha na kiasi kilichoombwa katika bajeti ya mwaka wa Fedha 2016/2017. Hali hii kwa kiasi kikubwa inaathiri utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Hata hivyo katika kipindi cha mwaka 2017/2018 bajeti ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Fungu 26) kwa ujumla imeongezwa kwa kiasi cha Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Sitini na Tano, Laki Nne Ishirini na Nne Elfu (1,265,424,000.00) ambalo ni ongezeko la wastani wa asilimia 25 na imepungua kwa Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tatu Themanini na Tatu, Laki Saba Kumi na Moja Elfu na Kumi na Moja (5,383,711,011) kwa Fungu 31 ambayo ni pungufu ya wastani wa Asilimia 26 Kama inavyoonyesha kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali Na.02: Tofauti ya Kiasi cha Fedha Kilichoidhinishwa 2016/2017 na Kinachoombwa 2017/2018 Katika Mafungu 31 na 26.**

| **Fungu** | **Fedha Iliyoidhinishwa 2016/2017** | **Fedha Inayoombwa Mwaka 2017/2018** | **Tofauti** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| 26 | Sh. 3,649,184,000 | Sh. 4,914,608,000 | Sh.1,265,424,000 | 25 % |
| 31 | Sh.20,386,699,448 | Sh.15,002,988,437 | Sh.5,383,711,011 | 26% |

## 6.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala yaliyobainika wakati wa uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Fungu 31 na Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais Fungu 26 kama ifuatavyo:

### 6.1 Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) - Fungu 31

i) Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati yaliyotolewa kwa Ofisi ya Makamu wa Rais mwezi Mei, 2016 na hasa hatua za

utekelezaji wa Mradi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, Luthuli Dar es Salaam. Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuendelea kufanya rejea ya ushauri na maagizo ya Kamati na kuyatekeleza kwa wakati.

ii) Kwa kuwa Serikali tayari ina Wakala wa Majengo (Tanzania Building Agency - TBA), ili kuokoa fedha za walipa kodi wa Tanzania; Kamati inashauri Ofisi ya Makamu wa Rais kuendelea kutumia ujuzi na utaalamu wa Wakala wa Majengo badala ya kutumia fedha za ziada kuwalipa wataalamu elekezi wengine kutoka Taasisi nyingine za kitaalamu kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa gharama za miradi hii.

iii) Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa kuendelea kuratibu vema masuala ya Muungano na hasa kwa kuwezesha kufanyika vikao vya kujadili masuala ya Muungano katika ngazi ya Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambavyo vilifanyika mwezi Januari 2016. Kamati inatoa Wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuendelea kuratibu vikao hivi katika wakati muafaka.

iv) Serikali itenge Bajeti ya kutosha na kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati hasa kwenye Miradi ya Maendeleo ili kuongeza kasi na kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo.

v) Serikali iendelee kutoa Elimu kwa Wananchi kuhusu umuhimu na faida zinazotokana na Muungano wa Pande zote mbili ili kuwawezesha Wananchi kuuthamini, kuupenda, kuudumisha na kuulinda Muungano huu kwa maslahi ya nchi yetu na kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

vi) Serikali iendelee kuchukua jitihada za dhati katika kutatua kero za Muungano ili kuongeza tija katika shughuli mbalimbali za biashara na maendeleo kati ya Tanzania Bara na Visiwani.

vii) Kwa kuwa uamuzi wa kuhamia Dodoma umeanza kutekelezwa na Serikali, Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuandaa mpango na kutenga fedha zaidi ili kukamilisha awamu zilizobaki za kuhamia Dodoma kwa wakati. Sambamba na hili, Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais kuandaa mpango wa Ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais katika mji wa Serikali hapa Dodoma.

viii) Kamati inatoa Wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kuandaa mpango wa Ujenzi wa Jengo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko Unguja na Ikulu Ndogo huko Pemba na kuhakikisha kwamba fedha kwa ajili ya Ofisi hizi inatengwa katika Miaka ijayo ya fedha.

ix) Kwa kuwa Ujenzi wa Jengo la Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais (Mradi Na.6309) lililopo Tunguu, Unguja umechukua zaidi ya miaka nane (8) kukamilika, kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kukamilisha jengo hili katika mwaka ujao wa fedha ili lianze kutumika kama ilivyopangwa.

x) Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushughulikia mapungufu mbalimbali yaliyoonekana katika mradi Na. 6389 wa ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Dar es Salaam na inaielekeza Ofisi ya Makamu wa Rais kushughulikia mapungufu yote ya kitaalamu yaliyoonekana katika jengo hili ili lianze kutumika mapema iwezekanavyo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya Ofisi .

xi) Kamati inaishauri Ofisi ya Rais Muungano kuendelea kuzingatia uwiano wa ajira Serikalini katika pande zote mbili za Muungano yaani, Tanzania Bara na Zanzibar uliokubalika na pande zote mbili , yaani uwiano wa asilimia **79:21**. Kamati inapongeza uamuzi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kufungua Ofisi za Sekretariati ya Tume ya Ajira Visiwani ili kutekeleza makubaliano haya.

xii) Ili kutekeleza vema majukumu na dhamana yake iliyopewa Kikatiba, Kamati inashauri kwamba, Tume ya Pamoja ya Fedha (*Joint Finance Commission*) ambayo imeanzishwa chini ya Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, isimamiwe moja kwa moja na Ofisi ya Rais au Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) na siyo Wizara ya Fedha na Mipango kama utaratibu ulivyo sasa. Hii itaboresha utendaji kazi na ufanisi wa Tume katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

## 6.2 OFISI BINAFSI YA MAKAMU WA RAIS (Fungu 26)

xii) Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais iendelee kuwezeshwa ili kumwezesha Mheshimiwa Makamu wa Rais kutimiza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha Kamati inaishauri Ofisi ya Hazina kuendelea kutoa fedha kwa wakati katika

Ofisi hii ili kuiwezesha ofisi kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na Maagizo mbalimbali kutoka Ofisi ya Rais.

xiii) Kwa kutambua umuhimu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Kamati inashauri fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais ziwekwe katika Mfuko Maalumu ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii na hasa majukumu ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 7.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Aidha, hatuna budi kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, umakini na umahiri mkubwa. Napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mheshimiwa January Yusuph Makamba (Mb), Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mhe. Luhaga Mpina, Mb, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais Prof. Faustine Kamuzora na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais(Muungano) kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa majadiliano ya pamoja kuhusu Makadirio na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Uzalendo na uchapakazi wao pamoja na ushirikiano mkubwa walionipa umesaidia kufanikisha kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. Ninaomba majina ya wajumbe wote wa kamati hii yaingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge (Hansard).

1) Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb, **Mwenyekiti**

2) Mhe. Najma Mutraza Giga, Mb, **M/Mwenyekiti**

3) Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb

4) Mhe. Ally Saleh Ally, Mb

5) Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb

6) Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb

7) Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb

8) Mhe. Seif Ungando Ally, Mb

9) Mhe. Ussi Pondezza, Mb

10) Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb

11) Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb

12) Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb

13) Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb

14) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb

15) Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb

16) Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb

17) Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb

18) Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb

19) Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb

20) Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb

21) Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb

22) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb

23) Mhe.Mathayo David Mathayo,Mb

24) Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb

25) Mhe. Juma Hamadi Kombo, Mb.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt Thomas D. Kashillah, Katibu wa Bunge, kwa kusaidia na

kuiwezesha Kamati kutekeleza Majukumu yake. Kipekee, nawashukuru makatibu wa Kamati Ndg. Angelina Sanga, Ndg. Stella Bwimbo, Ndg. Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndg.Raheli Masima kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa. Kipekee pia napenda kuishukuru idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.

**MWENYEKITI,**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

**24 Aprili, 2017**